***Muswada wa Bunge/sheria 195: Maelezo ya jumla***

Muswada wa Bunge 195/ Sheria ya Bunge(AB 195) una rekebisha vifungu vinavyo husiana na wanafunzi
ambao ni wasomi wa lugha ya Kiingereza. Iliidhinishwa na Gavana Steve Sisolak mnamo Juni 2, 2021, sheria AB 195 inaongeza haki za wanafunzi na wazazi wa wasomi wa lugha Kiingereza . Sehemu ya tatu ya
muswada au sheria uliojumuishwa hapo chini unatoa muhtasari wa haki hizi.

**Sehemu ya Tatu: Haki za wanafunzi na wazazi wa wasomi wa Lugha ya kingereza**

1. Mwanafunzi ambaye ni musomi wa lugha ya Kiingereza ana haki ya:
   a. Pokea elimu ya bure ya umma inayofaa bila kujali hali ya uhamiaji au lugha ya msingi ya mwanafunzi au mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi;
   b. Ufikiaji sawa wa programu na huduma zote zinazotolewa na shule au wilaya ya shule ambayo mwanafunzi amendikishwa kwa wanafunzi katika kiwango sawa cha daraja ambao sio wasomi wa lugha ya Kiingereza.
   c. Pokea mafunzo kwa kiwango sawa cha daraja kama wanafunzi wengine ambao wana umri sawa na mwanafunzi ambaye ni msomi wa lugha ya Kiingereza, isipokuwa kama shule au wilaya ambayo mwanafunzi ameandikishwa itaamua inafaa kwa mwanafunzi ambaye ni msomi wa lugha ya Kiingereza kuwekwa katika kiwango tofauti cha daraja;
   d. Ufikiaji sawa wa kushiriki katika shughuli kielimu za ziada ;
   e. Pokea huduma na misaada inaofaa ya kitaaluma iliyotolewa na shule au wilaya ya shule kwa wanafunzi waliojiunga na shule au wilaya ya shule ambao sio wasomi wa lugha ya Kiingereza;
   f. Kupewa mtihani kila mwaka ili kujua maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiingereza na kupata habari juu ya utendaji wa masomo ya mwanafunzi, pamoja na, bila kikomo, matokeo ya mtihani uliofanyika kulingana na NRS 390.105; na
   g. Kuendelea kuwekwa katika programu ya wasomi wa lugha ya Kiingereza kwa muda mrefu kama mwanafunzi ameainishwa kama msomi wa lugha ya Kiingereza isipokuwa mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi atakataa mwanafunzi kuwekwa katika mpango wa wasomi wa lugha ya Kiingereza.

2. Mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi ambaye ni msomi wa lugha ya Kiingereza ana haki ya:
   a. Kusajili/ kuandikisha mtoto wake katika shule ya umma bila kufichua hali ya uhamiaji ya mwanafunzi au mzazi au mlezi wa kisheria ;
   b. Kwa kadri iwezekanavyo, kuwa na mtafusili aliyehitimu mwenye kuongea katika lugha ya msingi ya mzazi au mlezi wa kisheria wakati mzazi au mlezi wa kisheria ana mazungumuzo ya muhimu sana pamoja na wilaya ya shule;
   c. Kwa kadri iwezekanavyo, pokea taarifa iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na lugha ya msingi ya mzazi au mlezi wa kisheria kwamba mwanafunzi amabaye ametambuliwa kama msomi wa lugha ya Kiingereza na atawekwa katika programu ya wasomi wa lugha ya Kiingereza;

d. Pokea habari juu ya maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiingereza na, ikiwa mwanafunzi ameandikishwa katika programu ya elimu ya lugha mbili, maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza lugha za programu hiyo;
e. Kwa ombi la mzazi au mlezi halali, onana na wafanyakazi wa shule ambayo mwanafunzi ameandikishwa angalau mara moja kwa mwaka, pamoja na mikutano mingine yoyote inayohitajika, kujadili maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiingereza;
f. Hamisha mwanafunzi kwenda shule nyingine ndani ya wilaya ya shule ikiwa shule ambayo mwanafunzi ameandikishwa kwa sasa haitoi programu ya Wasomi wa lugha ya Kiingereza au imewekwa kwenye mpango wa utekelezaji kulingana na sheria NRS 388.408;
g. Pokea habari inayohusiana na mtihani yoyote ya mwanafunzi kulingana na aya (f) ya kifungu cha 1; na
h. Wasiliana na Idara au wilaya ya shule, kama ifaavyo, ikiwa shule au wilaya ambayo mwanafunzi ameandikishwa anakiuka masharti ya sehemu hii.

3. Pamoja na vifungu vya aya (b) na (c) ya kifungu cha 2, bodi ya wadhamini ya kila wilaya ya shule itatoa habari kwa mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi ambaye ni msomi wa lugha ya Kiingerezakatika lugha na muundo ambao mzazi au mlezi wa kisheria anaweza kuelewa.
4. Kwa kadri iwezekanavyo, bodi ya wadhamini ya kila wilaya ya shule, kwa maandishi na kwa Kiingereza na lugha ya msingi ya mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi ambaye ni Msomi wa Lugha ya Kiingereza, itamwarifu mzazi au mlezi wa kisheria haki zilizoelezwa katika sehemu hii wakati wa kwandikisha mwanafunzi katika shule ndani ya wilaya ya shule au wakati mwanafunzi anatambuliwa kama Msomi wa Lugha ya Kiingereza.Wilaya ya shule itatoa nakala ya haki zilizoelezewa katika sehemu hii wakati wa usajili/ kwandikisha kwa kila mwaka wa mwanafunzi katika shule ndani ya wilaya ya shule kwa mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi ambaye ni msomiwa lugha ya Kiingereza.
5. Idara itatoa nakala zilizotafsiriwa za haki zilizoelezwa katika kifungu hiki katika lugha tano zinazojulikana zaidi ya Kiingereza inayozungumzwa kimsingi katika kaya/ familia zilizo katika kila wilaya ya shule, ambazo zinaweza kujumuisha, bila kikomo, Kihispania na Tagalog. Bodi ya wadhamini ya kila wilaya ya shule na kila shule inayosajili wanafunzi ambao ni wasomi walugha ya Kiingereza itachapisha nakala ya haki zilizoelezwa katika sehemu hii kwenye wavuti zao za mtandao kwa lugha nyingi iwezekanavyo, ambazo zinaweza kujumuisha, bila kikomo, na kama zinazotumika kwa wilaya ya shule, lugha zilizotafsiriwa na Idara kulingana na kifungu hiki.